# *Kutambulishwa Pamoja Na Kristo*

Asante, sana. Nina furaha sana kurudi, katika Jina la Bwana. Kidogo nimepwelewa na sauti, kwanza kabisa, lakini Bwana hunijalia kuingia kwenye gia ya pili, baada ya kitambo kidogo. Kwa hiyo, nimekuwa nikizungumza sana juma hili, mkutanoni. Pia kumekuwako na maswali mengi sana ya kujibiwa. Kisha ukitoka nje ya jengo, joto. Nalo . . . Sina homa mbaya. Wala kamwe sijajisikia mzima zaidi, maishani mwangu. Kwa hiyo, ninajisikia vizuri tu, ila koo langu limechoka tu. Nalo litakuwa sawa. Kwa hiyo ninataka kumshukuru kila mmoja wenu, kwa yote ambayo mmefanya.

2 Nilijaribu kutafuta . . . Wakati nikiendesha kuja huku, dakika chache zilizopita, Billy na baadhi yao walikuwa nje, wakijaribu kutafuta maskini ile familia iliyokuwa imeshuka huku na ikafilisika, wala haingeweza kurudi. Endapo wangali humu jengoni, ningependa kidogo . . . wangeinua mkono wao, ama kitu fulani. Ni—nilitaka kitu fulani juu ya hilo, mimi mwenyewe. Na kwa hiyo maskini hiyo familia inayotoka Michigan, ama mahali fulani, iliyo—iliyoishiwa na petroli ama kitu fulani, au pesa. Kama nyinyi—kama mngali hapa mjini . . . Mkiwaona baada ya mkutano, wapitisheni nyumbani kwangu. Mnaona? Ninataka kitu fulani katika hilo. Hiyo—hiyo ndiyo—hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa, ni kumsaidia, yeyote tuwezaye. Kwa hiyo, sasa, Bwana Yesu atubariki, ndilo ombi letu.

3 Sasa, hili limekuwa ni juma lisilo la kawaida, nasi tumekuwa na mambo yasiyo ya kawaida. Ila nitasema kwamba sijawahi kuona wakati ambapo Roho Mtakatifu alipata kutenda kazi kwa uhuru kuliko jinsi alivyofanya juma hili, kwenye ibada, imekuwa ni ajabu sana kwangu. Basi usiku ninapoingia, wakati mwingine ni saa saba usiku kabla sijaweza kulala. Ninashangilia tu katika mawazo ya Bwana Yesu kuwa mwema sana kwetu. Na sasa mimi . . .

4 Yeyote wenu watu mlio karibu na hapa, mjini, ama mlio majirani huku, msio na nyumbani bado, kanisa la nyumbani, mmekaribishwa hapa, kuja wakati wowote na kulifanya hili nyumbani kwenu. Kumbukeni, hatuna uanachama hapa, ni ushirika tu kwa wote. "Hatuna," kama Howard Cadle alivyozoea kusema, "hatuna sheria ila upendo; hatuna kanuni ya imani ila Kristo; hatuna kitabu ila Biblia." Na kwa hiyo sikuzote mmekaribishwa kwenye maskani hii ndogo.

Ambayo, tunatarajia, Bwana akipenda, mara tuwezapo, kujenga kanisa bora zaidi, ma—mahali pakubwa zaidi. Sio pakubwa sana, kwa kuwa tunaamini Yesu yuaja karibuni, wala hatutaki kitu cha gharama kubwa sana. Tunataka tu kitu fulani. . .Hili liko karibu kuporomoka. Limetumikia kusudi lake, nasi tunashukuru sana kwa ajili yake.

Kamwe sitasahau. Papa hapa ambapo mimbara hii imesimama sasa, yapata miaka ishirini na kitu iliyopita, nilipiga magoti kwenye kidimbwi cha kale, huku magugufarasi yakiwa juu ya kichwa changu. Ndipo Bwana akasema, “Jenga kanisa lako hapa.” Kwenye ploti ndogo, ambayo tulienda kwa Ingram na kuipata kwa dola mia moja na sitini, kama tungepajaza. Hiki kilikuwa ni kidimbwi cha barafu ambapo sisi sote tulitelezea.

5 Ndugu Jess Spencer anapaswa kukumbuka, hapa palikuwa ni kidimbwi hapa ndani, yeye na Dada Spencer. Nadhani mnakumbuka. Walikuwa wakileta farasi wanaokokota magari huku, na kuwazungusha *huku*, wasije wakatumbukia kwenye hicho kidimbwi.

Nilikuwa mvulana mdogo hapa kwenye Shule ya Ingramville. Hiki kilikuwa ni kidimbwi; tunatoka hapa nje na kuteleza kwa barafu, na—na kucheza hoki ya watoto na chochote kile, kwenye hicho kidimbwi. Ndugu Mike, unakumbuka wakati hiki kilipokuwa ni kidimbwi. [Ndugu Mike anasema, “Naam.”—Mh.] Naam, bwana. Ndugu Roy, huko nyuma.

Na sasa, mahali hicho kidimbwi kiliposimama, tuna sehemu yake tu iliyosalia, iliyo moja kwa moja *hapa* nyuma. Hapo ndipo tunapowabatizia watu majini kwa ondoleo la dhambi yao. Na sasa hii . . .

6 Mnajua, unapoyaleta maswali huku, na ambapo u—una kitu unachotaka kuwasilisha, na ni shida kwa sababu una kundi lililochanganyikana. Watu wamefundishwa njia moja au nyingine. Lakini wakati unapoweza kulielezea hilo jambo, hata kinyume na yale wamefundishwa, na utamu wa roho yao unarudi ukibubujika, huo ni utauwa, kwangu mimi.

Sitaki kuleta jina lolote lile. Lakini da—daktari fulani, kutoka nje ya mji, ndio kwanza akutane nami chumbani mle; daktari wa tiba, nadhani. Ndipo, akasema, kwa miaka kadha alikuwa amevurugika katika hilo. Alisoma kitabu kilichoandikwa kulihusu, kinyume na yale niliyokuwa nikifundisha. Lakini, kasema, tangu amekuwa akiketi mkutanoni, na kuona ukweli wa Maandiko ukiwekwa, lilitatuliwa milele.

7 Muda mfupi uliopita, nilikutana chumbani, na watu fulani kutoka nje ya mji, kutoka Illinois. Basi kulikuwako na yapata wahudumu wanne, wahudumu watatu ama wanne. Nao wakasema, “Ndugu Branham, tumefundisha kinyume, maisha

yetu yote, lakini tumeshika hilo ono sasa na kuona yaliyo Kweli hasa. Tumekuwa tukishangaa ilikuwa ni nini." Mnaona? Na sasa, hilo, mnaona, hivyo ndivyo tulivyo sasa . . .

8 Kile tu ilicho, ndugu, msifikiri hilo linalivunjia heshima kanisa lolote ama watu wowote. Hilo linaliinua tu Kanisa. Mnaona? Halafu basi, pamoja, hatuna budi kusimama. Hatuna budi kusimama pamoja. Wakati hao . . .

Hapo Mungu alipojigawa Mwenyewe kwenye Pentekoste, akiivunja ile Nguzo ya Moto katika nguzo ndogo sana za Moto, kisha akaenda na kuning'inia juu ya hao watu, naye Roho Mtakatifu akawajilia, kama Mungu alijigawa Mwenyewe miongoni mwetu, kila wakati mtu anapojiongezea kwetu, hiyo inaleta wengi zaidi kwenye Nguzo hiyo, wakati wote. Na pamoja, wakati likiwa ni Kanisa kuu la Mungu lililokombolewa, limevutwa pamoja, tutafanya safari kupitia angani, bila shaka kabisa.

9 Kamwe sijajaribu kuwatenganisha ama kupanda chuki miongoni mwa ndugu. Nimejaribu niwezavyo kuwa mwema niwezavyo, kuelewa. Na—na watu wengine, kama wao . . . makanisa yanayoudhamini mkutano wangu. Basi kama wao . . . Wanatofautiana mmoja na mwenzake, bali wananipenda, nao wataidhamini mikutano yangu. Nami ningekuja miongoni mwa watu wao, hakika nisingesema jambo moja. Mu—muungwana asingefanya hivyo, sembuse Mkristo. La hasha.

Halafu basi kama nikiwahi kufanya mikutano ya hema; ambayo ninawazia kufanya, Bwana akipenda, siku moja. Basi ni—nitaninii, kabla sijafundisha lolote la mafundisho haya, kwanza itakuwa ni ibada za asubuhi pamoja na wachungaji, kwa siku kadhaa, kuwajulisha yale ninayojiandaa kufundisha. Ndipo iwapo ndugu huyo halioni wala hakubali, ndugu yeyote, basi waache wachukue kusanyiko lao, waseme, "Sasa, siwataki msikie hili. Hatutahudhuria wakati wanapofundisha Hilo." Mnaona? Na kuwapa majaliwa. Daima tunataka kuwa katika uwiano na Mungu na pamoja na watoto Wake, pamoja na kila mtu.

10 Kwa hiyo, sasa, ninalo swali la kujibu usiku wa leo, Bwana akipenda. Nami niliwazia labda ningejibu swali hili, mapema tu. Nilidhani nilikuwa na lingine hapa, lakini ilikuwa ni ndoto ambayo mtu fulani alikuwa ametoa, naye alitaka niiombee na kutoa tafsiri yake. Ambalo, Bwana ameturehemu sana, kufanya hivyo, mara nyingi sana.

11 Sasa, tunawatakeni mjue, kabla hatujaanza katika ibada, ya kwamba nyote mmekaribishwa kwa furaha mrudi kwenye kila mkutano, kila tunapokuwa na mmoja. Na kutoka Louisville, kutoka nje ya mji, kutoka mjini na kote kote; wahudumu hawa wazuri; ndugu kutoka Sellersburg; wale waimbaji; yule mama, yeyote yule aliyekuwa, akiimba hapa nje, muda mfupi uliopita,

na huyo jamaa mdogo. Tunawashukuru tu, sana. Ni—nilikuwa nikizungumza na ndugu fulani huko nyuma, na hata sikupata nafasi ya kuona alikuwa ni nani, na kile ilichokuwa, bali hakika nilisikia. Nayo ilikuwa nzuri, na bila shaka ninathamini jitihada hiyo. Sasa tutaninii . . .

12 Niliikosa hii jana usiku. Mwanangu aliiweka mfukoni mwangu. Mtu fulani wa thamani alikuwa ameiandika. Na sasa kumbukeni, maswali haya si ili kuwa tofauti. Wakati mwingine, labda, wakati yanapoandikwa, yanasikika kama ni tofauti, lakini ni moyo mwaminifu ukijaribu kupata kujua. Mnaona? Hivyo ndivyo sikuzote tunavyolikaribia, mtu mwaminifu kweli akijaribu kupata kujua yaliyo kweli.

13 Sasa, hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa kwenye nyumba fulani, tukiwa na mkutano wa maombi. Naye Ndugu Junior Jackson, nilimsikia muda mfupi uliopita, ama nilifikiria nilimsikia, alikuwa pamoja nami. Naye alikuwa amemaliza kuzungumza. Ndipo palikuwapo na mhudumu kutoka kanisa lingine. Na mara niliposimama sakafuni, aliruka na kuanza, alitaka kubishana nami. Vema, ilitokea kulikuwako na yapata wahudumu watano pale, nao wote walikuwa wakitaka kumshambulia huyo mtu mara moja. Nikasema, "La. Msifanye hivyo. Sasa, yeye—yeye alinipa changamoto, basi acheni mimi na yeye tulijadili."

Vema, akaanza, "Sisi hunena ambapo Biblia inanena; tunanyamaza ambapo imenyamazia," na kadhalika. Nao hao wakaondoka. Basi katika dakika chache tu . . . Niliendelea kuandika Maandiko aliyokuwa akiyanukuu vibaya, kuyaweka mahali si pao. Kasema, "Hapakuwapo ila—hapakuwapo ila watu kumi na wawili waliopata kumpokea Roho Mtakatifu. Hao walikuwa ni wale mitume. Nao uponyaji wa Kiungu ulitolewa tu kwa hao kumi na wawili," na kadhalika. Kwa hiyo, mnaona, alikosa tu shabaha, kwa maili milioni moja. Kwa hiyo baada ya . . . baada ya mimi . . . Baada ya yeye kuzungumza kwa yapata nusu saa, nikamuuliza . . . Naye akasema mimi nilikuwa ibilisi.

14 Na kwa hiyo basi, alipomaliza kuzungumza, nikasema, "Sasa, jambo la kwanza ninalotaka kusema, ndugu, ninakusamehe hilo, kwa sababu hukumaanisha hilo. Ninajua hukumaanisha. Kwa kuwa, ikiwa wewe ni mhudumu nami ni mhudumu, inatupasa kuwa ndugu." Mnaona? Na kisha nikasema, "Sasa, kutokuelewana, katika Maandiko, ni jambo lingine."

15 Kwa hiyo basi tukaanza kuyachukua Maandiko. Ndipo maskini jamaa huyo alipotea sana, katika dakika moja, hakujua pa kusimama wala la kufanya. Halafu, alifungwa sana, hakujua la kufanya. Naye, alipotoka humo jengoni, hata hivyo, usiku huo, alisema, "Nitasema jambo moja, Ndugu Branham. Wewe una Roho wa Kristo." Mnaona?

Ndipo nikawazia, "'Ibilisi,' dakika chache zilizopita, na sasa 'Roho wa Kristo.'" Ni vile tu unavyolikaribia. Hivyo tu. Kristo hakuwa abishane.

16 Sasa—sasa, huyo mtu, kwa sababu kwamba alifanya hilo, mambo ya kutisha yalimpata; karibu aingie wazimu. Kutoka hospitalini ama kokote kule, aliruka kutoka dirishani, na nusura ajiue. Na sasa anarudi kwa baadhi ya marafiki zangu wema. Anatafuta, kila siku, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Anataka kuja nyumbani mwangu, apate kuwekewa mikono, ampokee Roho Mtakatifu; mhubiri wa kanisa kubwa la kimadhehebu. Mnaona?

17 Kwa hiyo, tunajibu maswali kwa uaminifu wa moyo, kwa yote tujuayo kujibu.

18 Na sasa nitalisoma swali hili, lililoandikwa vizuri.

1. **Ndugu Branham, waweza tafadhali kuelezea ni kwa nini watu katika Matendo 2:4 walinena kwa ndimi zingine ama lugha, hata kabla ya ule umati kukutana katika Matendo 2:6?**

Hilo ndilo swali la kwanza. Naam. Ni mtu yule yule, nadhani, pia. Naam, ni mtu yule yule.

19 Vema, sasa, kama utaona, ndugu, dada, yeyote yule aliyeliandika. Kamwe halikusema neno juu ya wao kushuka kwenye orofa ya chini, kutoka orofani. Wala lile kusanyiko halikuwa orofani. Lakini waliposhuka uwanjani ambamo umati ulikuwa umekusanyika, hapo ndipo walipowasikia wakinena kwa lugha. Mnaona? Mnaona?

20 Sasa, ungeweza kusema, "Vema, kweli walinena huko juu."

Na iwapo ilikuwa ni mjadala ama ubishi, ungekuwa vile vile na haki ya kusema, "Hawakunena mpaka waliposhuka hapa chini, kwa sababu, 'Sauti hii iliposikiwa.'" Mnaona?

Sasa, jambo lingine hapa, linaambatana moja kwa moja nalo.

2. **Waweza kueleza jinsi ambavyo Simoni alijua Roho Mtakatifu alikuwa ametolewa katika Matendo 8:18? Hiyo ni huko Samaria.**

21 Vema, kunalo jambo moja, yeye hakujua walikuwa na Roho Mtakatifu kwa sababu ya kunena kwa lugha, ama Biblia haikusema walinena. Waliona tu matokeo. Hakuna mtu anayeweza kumpokea Roho Mtakatifu pasipo jambo fulani kutukia kwao. Hiyo ni kweli. Ila haikusema walinena kwa lugha pale, kwa hiyo hapana shaka lilikuwa ni jambo lingine aliloona mbali na kunena kwa lugha, kwa sababu kamwe halikutaja wao wakinena kwa lugha.

3. **Pia eleza tunajuaje baadhi ya watu kwenye Siku ya Pentekoste walinena Kigalilaya.**

22 Sehemu kubwa yao kule ilikuwa ni Wagalilaya. Nao hao wote. . .Sasa, kama nilivyosema asubuhi ya leo. . .Sasa,

kunayo mambo mawili, maoni mawili. Sasa, nitachukua upande kwamba hao watu walikuwa wakinena kwa lugha; hao watu wakinena sio kwa ndimi, bali kwa lugha, walipotoka kwenye chumba cha juu na kuanza kukutana na watu. Lakini iwapo utayasoma Maandiko, sikiliza kwa makini sasa.

. . .*hawa wote si* Wagalilaya ambao wananena?

*Imekuwaje—imekuwaje sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?*

. . .*hawa wote si* Wagalilaya wanaonena?

23 Huenda walikuwa wakizungumza Kigalilaya, bali wao walikuwa wakiwasikia katika lugha nyingine. Huenda ikawa walikuwa wakizungumza lugha nyingine, lugha yao wenyewe. Mojawapo, haingejalisha; lingali haliifanyi dhana ya Kipentekoste sahihi. Mnaona? Maana. . .Sikilizeni. Sababu yake ndiyo hii. Sio kusema jambo tofauti, bali kuufafanua ukweli. Kama ukiangalia, kwa nini Petro akasimama basi na kuuhutubia umati wote, nao kila mmoja akamsikia katika lugha aliyokuwa akinena. Kwa kuwa, elfu tatu waliongoka, Wayahudi waaminifu waliokuwa wamezama katika dini yao walivyoweza kuzama. Lakini hapana shaka walisimama, wakaelewa kila neno, la Petro akihubiri juu ya manabii, na kadhalika, akiwaleta kwenye Pentekoste. Kwa kuwa walipaza sauti, na kusema, "Waume na ndugu zetu, tufanye nini tupate kuokolewa?"

Petro akasema, "Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi yenu."

24 Sasa hebu niseme tu hili, kwa—kwa ninii. . .moyo wangu wote, kusudi mpate kuona ninii. . .kile ninachojaribu kuwaelezea. Bila shaka ninaamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini ya kwamba ni karama kwa Kanisa. Ninaamini ya kwamba kuna lugha. Nimenena kwa lugha, mara nyingi, mimi mwenyewe.

25 Hebu niwape mfano mdogo, kile ninachofikiri Pentekoste ilikuwa. Halafu nitaninii. . .kitu fulani kama hiyo, sasa, ama kitu fulani cha jinsi hii. Nilikuwa huko Dallas, Tex-. . .Houston, Texas, kabla tu ya picha *hii* kupigwa, yapata siku moja. Tungalipata ule Ukumbi wa Muziki; tulikuwa na watu elfu nane. Hao watu wasingeweza kuingia, kwa hiyo tukaenda kwenye maskani ya Raymond Richey. Ninasahau tu. . .Ilikuwa ni maskani kubwa, kubwa mno. Na—nasi tukaijaza hiyo kabisa. Nami ningehubiri na kuwaombea wagonjwa, hapa. Ndipo, wakati wakiwatoa nje, ningeenda kule, na kuhubiri na kuwaombea hapa, kwa Raymond Richey, ng'ambo ya mto.

26 Ndipo basi tulipokuwa kule, tukijiandaa kurudi kwenye Ukumbi wa Muziki, Mimi. . .Howard alikuwa ameniacha niende kadiri nilivyoweza kwenda. Ndipo akanigusa begani, akanipigapiga ubavuni. [Ndugu Branham anajipigapiga—Mh.]

Kama mliona, humo chumbani, upako unapokuwapo, watanipigapiga, namna *hii*. [Ndugu Branham anajipigapiga—Mh.] Hiyo inamaanisha, “Wakati wa kuondoka umewadia. Usiseme zaidi. Hima.” Naye Howard, ilikuwa, ningesimama pale, yeye angeushika tu mkono wangu, anitupe begani mwake na kutoka nje. Mnaona? Maana, yeye alijua nilikuwa nimefanya ya kutosha.

Vema, nikaanza kuondoka jukwaani wakati aliponipapasa. Nikasema, “Sawa, ndugu.” Nikaanza kuondoka jukwaani, ndipo msichana, msichana mdogo, alikuwa ameketi, amesimama hapa, akilia. Msichana mdogo, wa Kimeksiko, alionekana mwenye umri wa miaka kumi na miwili, kumi na minne, tineja tu. Ndipo nikamwangalia, nami nikasema, “Kwani kuna nini, kipenzi?” Nikasema, “Analia, Howard, kwa sababu. . . ”

Kasema, “Umefanya ya kutosha. Unalo kundi lingine kule, linalongojea.”

Ndipo nikasema, “Mlete hapa.” Nami nikanyosha tu mkono, nikamwashiria *hivyo*. Ndipo akaja jukwaani. Ninaamini Ndugu Wood na hao wengine walikuwako, sasa. Walikuwa mkutanoni. Sijui kama ni kwenye wakati huo au la. Ndugu Wood, uko wapi, usiku wa leo? [Ndugu Banks Wood anasema, “Hapa.”—Mh.] Alikuwa. . .Hiyo ni kweli? [“Kweli.”] Naam, ulikuwako. Ndipo nikasema, “Mlete hapa jukwaani.”

Vema, nikasema, “Angalia, kipenzi. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako?” Naye akaendelea tu kuinamisha maskini kichwa chake. “Vema,” nikawazia, “Huenda akawa ni kiziwi na bubu.”

27 Kwa hiyo, nikaangalia tena. Nikaona ilikuwa ni mazungumzo. Ndipo nikasema, “Loo, hawezi kuzungumza Kiingereza.” Asingeweza kuzungumza Neno moja la Kiingereza. Kwa hiyo alikuwa ametoka Meksiko. Kwa hiyo wakamleta mfasiri. Basi nikasema, “Unaamini, kipenzi, ya kwamba Bwana Yesu anaweza kuniambia shida yako ni nini?”

Vema, akamjibu yule mkalimani, akasema, “‘Naam.’ Aliamini.”

Ndipo nikasema, “Unaweza kuzungumza Kiingereza, hata kidogo?” Naye mkalimani akamfasiria.

Akasema, “La.” Kamwe hakujua maneno yoyote ya Kiingereza. Alikuwa ni wa kutoka Meksiko. Na kwa hiyo wakati mimi. . .

28 Ndipo ono likaanza. Nami nikasema. . .Hawafasiri ono, mnaona, maana unazungumza ukiendelea. Kamwe hawalifasiri ono, hivyo, mpaka lote limekwisha, halafu basi wanawaambia kilichotukia. Kwa hiyo, basi, wakati nilipoanza kuzungumza, niliona ono. Nikasema, “Ninamwona msichana mdogo wa yapata umri wa miaka sita. Yuna nguo nene, isiyo laini, mwenye

ukili wa nywele ukining'inia mgongoni mwake, na vifundo vya utepe juu yake. Amekete karibu na mekoni pa mtindo wa kale. Kuna birika kubwa, naye anakula mahindi ya manjano kutoka kwake. Anakula mahindi mengi sana hata anaugua vibaya sana. Anaanguka, naye mama yake anamlaza kitandani, naye anashikwa na vipindi vya kifafa. Na hicho ndicho kilichompata. Mnaona?" Nikasema, "Umekuwa na kifafa, tangu wakati huo."

Ndipo upesi, kabla mtu yeyote hajasema lolote, akamwangalia mkalimani, akasema, katika lugha yake mwenyewe, "Nilidhani yeye asingeweza kuzungumza Kihispaniola."

Naye mfasiri akasema, "Kwani ulizungumza Kihispaniola?"

Nikasema, "La, bwana. Nilizungumza Kiingereza."

Akasema, "Vema, yeye alisema ulizungumza Kihispaniola."

Nikalishika. Nikasema, "Hebu zimeni vinasasauti." Kulikuwako na lundo kubwa la vinasasauti, labda thelathini vikiendelea, siku hizo.

Ndugu Roy Roberson, si ulikuwa huko? [Ndugu Roy Roberson anasema, "Naam."—Mh.] Naam. Ndugu Roy Roberson, na Dada Roberson na hao wengine, walikuwapo.

29 Kwa hiyo nikasema, "Zimeni vinasasauti. Vifungulieni tena." Nacho kilikuwa kabisa ni Kiingereza. Lakini, mnaona, ndipo wakati nilipoanza . . .

Mradi tu hilo ono lilikuwa likiendelea, mimi nilikuwa nikizungumza Kiingereza ila yeye alikuwa akisikia katika Kihispaniola. "Imekuwaje sisi kusikia kila mtu lugha yetu, tuliyozaliwa nayo?" Mnaona? Na, lakini, mara nilipoanza kuzungumza, mimi mwenyewe, basi hakusikia kitu chochote nilichosema. Lakini wakati ule uvuvio ukiwapo . . .

30 Sasa tumia hilo kwenye Pentekoste, mara moja tu. Mnaona? Rafiki, Mungu ndiye hakimu wangu. Roho Mtakatifu alifanya hilo. Sasa hebu tutumie hilo huko nyuma kwenye Pentekoste, tupate maana yetu. Roho Mtakatifu asingefanya lolote ku—kusema tu alililifanya. Inabidi pawe na chanzo na sababu. Mnaona?

31 Sasa, kwenye ile Siku, "Imekuwaje sisi kusikia kila mtu lugha yetu, tuliyozaliwa nayo? Hawa wote, wanenao, si Wagalilaya?" Walijuaje walikuwa ni Wagalilaya, endapo hawakuwa wakizungumza Kigalilaya? Wote walivalia vile vile. Walijuaje walikuwa ni Wagalilaya? "Hawa wote, wanenao, si Wagalilaya? Basi imekuwaje sisi kusikia kila mtu, lugha yetu, tuliyozaliwa nayo?"

32 Ndipo, mtu mwingine anasimama, Mgalilaya, Petro, na kuanza kuwahubiria. Na kwa njia moja au nyingine, katika umati huo wa watu, watu elfu tatu walimwelewa, nao wakaja na kuongoka, na kuyatoa maisha yao kwa Kristo.

33 Sasa sikilizeni. Hebu niwapeleke tu kwenye Andiko moja zaidi, tafadhalini. Hebu tumwendee yule Mtakatifu mashuhuri Paulo, kisha tutasoma mlango wa 12 wa Wakorintho wa Kwanza. Kisha tushuke kwenye mlango wa 13 wa Wakorintho wa Kwanza, wakati Paulo akizungumza juu ya, "Kama masikio yakiiambia pua, 'Sina haja na wewe,'' na kadhalika, viungo vya ule Mwili. Halafu katika mlango wa 13—wa 13, sikilizeni yale aliyosema sasa.

34 Sasa, tunajua ya kwamba kuna aina mbili za lugha zilizotajwa katika Biblia. Moja ya hizo ni lugha, ambayo ni—ni lahaja ya duniani. Sasa, hiyo nyingine ni lugha isiyojulikana.

35 Sasa, wengi wa watu wangu wa thamani sana... Nimewaambia ya kwamba mimi ni Mpentekoste. Sasa, wengi wa watu wangu wanaamini ya kwamba, ya kwamba, wanapompokea Roho Mtakatifu, wao wanasimama tu na kunena kwa lugha isiyojulikana. Hiyo ni kinyume kabisa na Maandiko. Basi watu hawajui yale wanayosema. Lakini, kwenye Siku ya Pentekoste, kila mmoja alijua yale waliyokuwa wakisema. Hiyo ilikuwa ni kwenda, kwenye kila taifa. Mnaona? Yesu alisema, "Injili hii haina budi kuhubiriwa ulimwenguni kote, kuanzia Yerusalemu." Hapo ndipo ilibidi iwe hivyo.

Sasa angalieni. Paulo alisema, ya kwamba, "Lugha moja, ambayo, kama uliinena, lugha isiyojulikana ambayo ni karama ya lugha, isipokuwa iwe kwa tafsiri ama kwa ufunuo, kwamba haitafaidi sana."

Halafu tunaona, kwamba, katika mlango wa 13, yeye alisema "Nijaponena kwa lugha za wanadamu," hizo ni lahaja za duniani, "ama za Malaika. Nijaponena kwa lugha za wanadamu ama za Malaika, wala sina upendo, si kitu mimi." Kwa hiyo ungeweza kunena kwa lugha halisi za wanadamu na Malaika pia, na hata hivyo huna Roho Mtakatifu.

36 Si tulikuwa nalo, katika Waebrania 6? "Mvua ilinyea ngano na magugu pia." Hivi Yesu hakusema, "Mvua huwajia wenye haki na wasio haki"? Mnaona? Mvua ile ile inayoifanya ngano kukua, ndiyo mvua ile ile inayoifanya ni—ninii . . . kukua. Lakini, kwa matunda ya hiyo, mnaijua.

Nalo tunda la kwanza la Roho ni upendo. Yale Paulo aliyosema, "Kama nina—kama nina zote, ninaweza kunena kwa lugha za kila namna, wala sina upendo, uvumilivu, upole, imani, subira, na kadhalika, hainifaidi kitu." Mnaona?

37 Halafu angalieni kuhusu karama. Mnasema, "Loo, yule *pale* mtu mashuhuri wa Mungu. Loo, yeye anafanya miujiza." Hilo bado halimfanyi sawa.

38 "Nijapokuwa na karama ya miujiza," Paulo alisema, katika Wakorintho wa Kwanza, kitu kama hicho, "nijapokuwa na imani kiasi cha kuhamisha milima, wala sina matunda hayo ya Roho,

upendo, ningali si kitu mimi.” Mnaona? Hakika, imani itafanya chochote.

Hiyo ndiyo sababu sikuzote mimi husema “Huponywi kwa ustahilifu wa wokovu wako. Ustahilifu wako. . .unaponywa na ustahilifu wa imani yako, ‘Kama unaweza kuamini.’”

39 Sasa, angalieni, “Nijaponena kwa lugha za wanadamu na Malaika, wala sina upe-. . .,” ingawa angeweza kufanya hivyo, “Si kitu mimi.” Kwa hiyo, unaona, huwezi kusema kitu.

40 Sasa, kwa rafiki yangu wa thamani wa Methodisti. Nina wawili wanaoketi papa hapa, na kila mahali. Ninao hapa nje, wengi wao. Kanisa la Methodisti lilikuwa likiamini, nyuma katika siku zake za mwanzoni, siku za kale, kwamba, “Mtu anapokuwa na dini ya kutosha, na ametakaswa, kupiga makelele, alikuwa Naye.”

Pentekoste ilisema, “Aliponena kwa lugha, alikuwa Naye.”

Na siku hizi, wanasema, “Endapo una huduma ya uponyaji, unaye.” Bali hakuna yoyote ya. . .

41 Sikiliza, rafiki. Usijaribu kutegemea na kutafuta mihemko. Badala yake, tegemea uhalisi, unaona, sio mhemko. Kupiga makelele ni sawa. Kunena kwa lugha ni sawa. Kumsifu Bwana ni sawa. Imani kwa ajili ya miujiza ni sawa, mambo hayo yote.

42 Na hisia hizo, baadhi yao husema, “Loo, nilimsikia kama upepo ukienda kasi.” Mwingine anasema, “Nilihisi Moto nafsini mwangu.” Ati nini? Hilo halililifanyi sawa, vyovyote vile. Ni kile ulicho ukiisha kumpokea, unaona, hilo ndilo muhimu. Unaona? Kwa hiyo huwezi kulisukumia mhemko wowote ule.

43 Sasa, hivyo ndivyo vizuri sana nijuavyo kwa uaminifu. Sasa, huenda nikakosea; kama nimekosea, basi nimeyaelewa Maandiko vibaya. Na kama ni kinyume, vema, simaanishi kuwa kinyume. Mnaona? Lakini ninaelezea tu masimulizi yangu ya yale ninayoamini kwamba ni kweli.

44 Sasa, tumechukua wakati wetu mwingi juu ya hili, kabla hatujaanza ibada ya kawaida. Na sasa—sasa, hatuyataji mambo haya mara nyingi sana maskanini, wakati mwingine. Hii imekuwa ndiyo mara ya kwanza, nadhani, kwa muda mrefu, kwa labda mwaka mmoja ama miwili, ama kitu fulani. Na halafu labda baadhi ya watu wetu waingie, nao wanasema, “Vema, Ndugu Branham, ni—nimekuwa na midomo migeni. Nami nimefanya *hivi*. Nimefanya *vile*.”

Nimesema, “Vema, sawa. Hilo ni jema sana.”

45 Sasa, ukitaka kunena kwa lugha isiyojulikana, ninaamini Mungu atakuruhusu kufanya hivyo. Lakini kulingana na Maandiko, ungali si kitu mpaka Roho Mtakatifu aje.

Ndipo, Roho Mtakatifu akiisha kuja, basi unaweza kunena kwa lugha na kuwa na. . .Mungu atachukua tu asili yako,

na kukukatia, na kukufanya mtumishi bora zaidi unavyoweza kuwa. Huenda akakufanya uihubiri Injili. Huenda akakufanya uwe na karama ya kunena kwa lugha. Huenda akakufanya nabii. Huenda akakupatia roho wa unabii. Anaweza. Ni vigumu kusema, yale atakayokufanyia. Ama, huenda akakufanyia mambo hayo yote. Lakini jambo la kwanza, ni kuwa na hakika, ya kwamba, "Kwa ninii moja. . . " Sio mhemko. "Bali kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Halafu basi hizo karama hutoka kwenye Mwili huo, mnaona, kunena kwa lugha na kila kitu.

46 Jambo ni kwamba, kama—kama Mnazarayo akinijia. Mngesema, "Ndugu Branham, sasa, huyo hapo Mnazarayo na Mmethodisti. Wanasema walimpokea Roho Mtakatifu wakati walipopiga makelele. Walisema walimpokea Roho Mtakatifu." Sisemi hawakumpokea.

Lakini hili hapa jambo moja ninaloangalia, "Kwa tunda lao."

Ukweli unapofunuliwa, baadhi yao huupinga, kwa ukali, "Huyo ni ibilisi." Halafu, hilo tunda linaonyesha mahali lilipotoka. Mnaona? Inaonyesha hawakumpata. Lakini wale walio tayari kutembea katika Nuru, wanalipokea Neno.

47 Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa nikihubiri huko chini Kentucky. Ndipo nje ya huo mkutano, kulikuwako na mtu wa kanisa linaloamini kwamba siku za miujiza zimepita. Alikuwa ameshika fanusi mkononi mwake. Naye akasema, "Nilikungojea tu, mhubiri." Mimi pamoja na mjomba mzee, ambaye ametuacha sasa.

Nami nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Mimi ni *fulani-wa-fulani*."

Ndipo nikamsalimia kwa mkono. Nikasema, "Hakika nina furaha kukutana nawe, ndugu yangu."

Naye akasema, "Ninataka tu kukwambia ya kwamba ninaamini kwamba umekosea kabisa."

Nikasema, "Vema, una haki ya kufanya hivyo, kwa sababu wewe ni Mmarekani." Naye akasema. . .Vema, unaona, nasi tuna. . .Nikasema, "Kukosea juu ya nini? Unamaanisha juu ya uponyaji?" Nikasema, "Vipi kuhusu msichana yule mwenye miguu mitupu ambaye ndio kwanza atembee pale jana, jana usiku, aliyekuwa na mtoto mchanga?"

Hakuwa na zaidi ya umri wa miaka kumi na minne, mwenyewe, miguu mitupu. Maskini. . .Mnaiitaje hiyo? Ginghamu, kaliko, ama namna fulani ya nguo. Sijui mambo ya vitambaa. Na—naye alikuwa na mtoto mchanga mkononi mwake, ndipo akanijia. Huku watu wamesongamana madiri-. . . Nalo hili lilikuwa ni kanisa la Methodisti, kanisa la Methodisti la Kilima Cheupe, nje tu ya Burkesville, Kentucky, nilikozaliwa.

Naye alikuwa amemshika maskini mtoto huyu mchanga. Basi nikasema, "Dada . . . "

Nilikuwa nimeuliza, "Kuna mtu yeyote mgonjwa?"

Ndipo akapanda kuja pale, maskini, mama mwenye haya, amekiinamisha maskini kichwa chake. Naye akasema, "Naam, bwana, mtoto wangu mchanga." Naye maskini mtoto huyo alikuwa akienda *hivyo*.

Nikasema, "Ana shida gani, dada?"

Akasema, "Ana mikutuo."

Nikasema, "Ati mikutuo?"

"Naam, bwana."

Nikasema, "Amekuwa na mikutuo hii muda gani?"

Naye akasema, "Vema, tangu alipozaliwa, naye ana umri wa karibu mwaka mmoja."

Nami nikasema, "Uko tayari kuniruhusu nimshike mtoto huyo mchanga?" Huku juu milimani kidogo inakubidi kuangalia jambo hilo.

Naye akasema, "Naam, bwana." Akamweka huyo jamaa mdogo mkononi mwangu.

48 Moyoni mwangu, nilisimama tu kimya, kwa dakika moja. Nikasema, "Mungu, kama utanijalia kuwavuta watu hawa, basi nifanyie jambo fulani sasa."

Ndipo nilipokuwa nimemshika mkononi mwangu, aliacha kukutuka. Nikamwangalia. Nikamweka, mikononi, nikacheza naye, naye akatabasamu na kunicheka. Nikamwangalia huyo mama. Naye akainua . . . Huku amekiinamisha kichwa chake chini, nywele zimetenganishwa na zinaning'inia mgongoni mwake, na zina misokoto. Akakiinua kichwa chake, huku machozi yanatiririkia maskini mashavu yake. Wanaume wakali wamesimama pale, masharubu usoni mwao, marefu *hivi*, na machozi yanatiririka mashavuni mwao. Nikaangalia kote. Nikasema, "Huyu hapa mtoto wako mchanga, dada. Yesu Kristo anamponya." Ndipo hao wanawake wazee wakaanza kuzimia na kuanguka sakafuni, na kuwamwagilia maji usoni mwao, na kuwapepea.

Na—na, mbona, nikasema, "Ni kitu gani kilichosababisha hilo?"

Akasema, "Bw. Branham, siwezi kukubali chochote mpaka nimekiona waziwazi kabisa."

Nikasema, "Vema, wazo zuri, nadhani. Lakini," nikasema, "nataka kukuuliza, unaishi wapi wewe?"

Akasema, "Huku ng'ambo ya mlima hapa, mbali. Karibu nyumbani pamoja nami kwa chakula cha jioni, nami nitakupa maziwa ya mtindi na ugali."

Nikasema, "Ningependa kwenda, na nina njaa kweli, lakini," nikasema, "siwezi kuja. Sina budi kwenda nyumbani na mjomba wangu." Naye. . .Nikasema, "Vema, ninataka kukuuliza—ninataka kukuuliza jambo fulani. Unajuaje utafika nyumbani?"

Akasema, "Vema, nitaenda tu ng'ambo ya ule mlima."

Nikasema, "Je, unaweza kuona nyumba yako?"

Akasema, "La."

Nikasema, "Basi unajuaje utafika kule?"

Akasema, "Kunayo njia ya miguu inayoelekeza."

Nikasema, "Lakini, hata hivyo, huwezi kuiona. Nawe ndio kwanza uniambie usingeweza kukubali chochote isipokuwa ukione, dhahiri sana."

"Loo," akasema, "Nitachukua tu hii nuru na kuenenda nuruni."

Nikasema, "Hilo ndilo tu ninalojaribu kukufanya ufanye."

Kadiri tu hiyo fanusi inavyotoa nuru, wewe enenda Nuruni kama Yeye alivyo Nuruni. Tutafika kule basi. Ingawa siuoni ule mwisho, dhahiri, lakini ninajua utakuwako.

Na tuombe sasa.

49 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya wema wa Yesu Kristo, ambaye Ndiye kiini cha upendo. Nami nilikuwa nikiwazia ya kwamba Wewe umenikasirikia, bali Yesu alinipenda. Lakini ninaona sasa ya kwamba Yesu ndiye moyo wenyewe wa Mungu, kwa hiyo na—najua kwamba unanipenda na—na uliteseka kwa ajili yangu.

50 Na, Baba Mungu, ninauombea ulimwengu huu leo hii, na nchi yetu. Ninaomba, Bwana, msamaha wa makosa yangu mwenyewe na wa makosa ya watu wangu, watu ambao Wewe umenipa kuwachunga. Nami ninaomba ya kwamba utawabariki, na kila mmoja wa watu ambao wamekuwa kwenye mkutano huu mdogo, ambao waliuliza maswali. Ama—ama, labda nimesema jambo fulani kinyume na yale wanayoamini. Bwana, siwezi kulielezea, mimi mwenyewe. Siwezi. Lakini jalia. . . Je, utawajalia tu kujua, Baba, ya kwamba moyoni mwangu, yale ninayomaanisha? Tafadhali. Ninaomba utafanya hivyo. Wabariki, pamoja.

51 Tubariki sasa wakati tukilingojea Neno Lako, dakika chache tu kabla ya ibada ya ubatizo. Tusaidie kunena yaliyo kweli. Tusaidie, katika Ujumbe huu usiku wa leo, koo langu likiwa kidogo limepwelea. Ninaomba ya kwamba utanisaidia, Mungu mpendwa, na hata utawaponya wagonjwa na wanaoteseka walio miongoni mwa hawa watu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

52 Sasa, mkiweza, kwa dakika chache tu zijazo, na tufungue Kitabu cha Warumi, mlango wa 6.

Loo, ngojeni. Ninaamini nina ninii. . .Aisee, nina lundo kubwa zaidi la mas-. . .Aisee, nitayajibu tu haya Jumatano usiku, kama hilo ni sawa. Nimemaliza, saa imeenda sana sasa. Sikuona hayo yamewekwa hapo mpaka sasa hivi.

Sasa, Warumi, mlango wa 6, hebu tusome.

> *Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?*
>
> *Hasha. Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?*
>
> *Hamfahamu ya kuwa sisi sote. . .tuliobatizwa* katika *Yesu Kristo tulibatizwa* katika *mauti yake?*
>
> *Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo* katika *mauti yake: kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa nia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*
>
> *Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake.*

53 Kama ningechukua somo usiku wa leo, kwa yapata dakika ishirini, ningesema jambo hili, "utambulisho," *Kutambulishwa Pamoja Na Kristo.*

54 Mnajua, kunao, nchini siku hizi, watu wengi sana wasioridhika. Pia inashangaza, unapotembea huku na huku na kuona kutoridhika kwingi sana. Watu karibu hawajui wanalotaka kufanya. Wanashuka barabarani yapata maili sabini na themanini kwa saa, kwenye eneo la maili thelathini; wanafunga breki na kupiga kona, na kuanza kwa spidi kubwa sana hata wanaunguza tairi zao nusu, kwenda bloku moja ya mji, ili kuketi na kuzungumza kidogo. Inaonekana kana kwamba watu hawajui wanachotaka.

55 Wengine wao wanasumbuka sana hata wanashuka kwenye duka la dawa na kujinunulia chupa ya aseniki, tindikali ya salfuriki ama kitu fulani, na kujiua. Wanawakuta wamelala mauti. Wengine watafungulia mabomba ya gesi chumbani, ama kuketi kwenye magari yao pamoja na bomba la gesi ya kaboni monoksaidi, wakijaribu kuyaondokea maisha. Baadhi yao watapanda kwenye daraja, na kuandika muhtasari mdogo na kuubandika kotini mwao, na kuuweka chini, kisha wanajitumbukiza hata kufa mtoni; wanaruka kutoka milimani, minara mirefu. Na wengine watachukua bastola na kuilenga kichwani mwao, na kwa kweli wazilipue bongo zao. Ni kwamba tu hawaridhiki.

56 Hospitali zimejaa watu wasioridhika. Hospitali za wendawazimu zimejaa pomoni. Kutoridhika! Hawajui

watakacho. Inaonekana kuna kitu wanachotafuta, bali kamwe hawakifikii.

57 Na pia tunaona ya kwamba, nyumba, ambazo ndizo uti wa mgongo wa taifa na—na wa kanisa, tunaona nyumba zimevunjika, na mahakama za talaka zimefurika na talaka. Uhalifu wa vijana, wa—wa akina mama wakiwaacha watoto wao wadogo na mayaya na—na kuondoka, kwenda kazini na mahali fulani, wakati waume zao wana kazi nzuri, lakini kamwe hawaridhiki kuwa mama na kukaa nyumbani. Hawaridhiki kuvaa kama wanawake wa heshima. Wa—wanataka kuvaa kama wanaume. Wanaume wanataka kuwa kama wanawake. Nao wananinii tu. . .Inaonekana tu kuna kasoro fulani, mahali fulani. Nao watu wanatafuta kitu fulani, wala hawawezi kukipata. Hiyo ni hali ya kusikitisha kuwa ndani yake.

58 Wametafuta kila mahali, kupata kitu fulani, kujifanyia mfano. Hebu tuwachukue wanawake wa siku zetu, wataangalia televisheni mpaka wamwone bingwa fulani wa sinema. Ama, atatoka nje, amevalia kwa njia fulani, ndipo wanawake wote watataka kuvaa kama yeye, ama kutenda kama yeye, kumfanya yeye mfano. Baadhi ya wasichana warembo, katika upeo wa maisha, watajaribu kujifananisha wenyewe, na kujaribu kumfanya bingwa fulani wa sinema mfano wanaopaswa kuufuata. Ndipo hatimaye wanajikuta wameishia kwenye tundu la dhambi ambamo hawawezi kutoka. Ni chukizo jinsi gani! Kuwaona wakija mkutanoni, machozi yakitiririka mashavuni mwao, bali wanatafuta kitu fulani.

59 Hebu tuwachukue wanaume. Wanaume, unawakuta mtaani ama katika biashara zao. Mzee anataka kuwa tineja. Atakata nywele zake, mtindo bapa, na kufanya m—mkiabata upande wa nyuma. Anataka kuwa tineja. Tineja anataka kuwa kama mmoja wa hawa wafalme wa roki. Wanaishia wapi? Katika dhambi na aibu.

60 Mwanadamu anaonekana kutoridhika. Anakimbia kila mahali. Watachukua. . .watasikiliza redio, wapate utani na vitu ambavyo hawa wafanya mizaha wanatoa. Nao watatoka waende wakajaribu kuwaiga ama—ama kutenda kama watu hao.

61 Hebu mchukue mvulana mdogo mtaani. Jinsi ninavyojua hilo! Naye hana budi kuwa Paladin, ama Hopalong Cassidy. Ama. . .Nao ulimwengu wa biashara unashika hilo na kujipatia mamilioni ya dola kutoka kwake. Hawana budi kuwa Roy Rogers, ama—ama Bw. Dillon, ama—ama nyota fulani wa kipindi cha televisheni.

Wanajaribu kumwiga mtu huyo. Wanawaweka kama mfano. Wamewachukua kama kigezo cha—chao cha maisha. Nao wanapata nini mwishoni mwa safari? Maskini jamaa hao wadogo wanageuka kuwa majambazi na wezi. Hao wanawake wanageuka kuwa makahaba, na—na wazurura mitaani, na—na

watu wahalifu. Wanaume wanageuka kuwa wacheza kamari, na, "Wapenda anasa kuliko kumpenda Mungu." Makanisa yanajaribu kuiga kanisa lile lingine, lile kanisa kubwa.

62 Inaonekana tu tunaona, hakuna utoshelevu miongoni mwa watu. Ni nini wao . . .

Ni kitu gani kinachowafanya kufanya hivyo? Ni kwa sababu fulani. Ni maumbile. Mungu aliwapa asili hiyo. Wanayo asili inayowafanya wapende kuwa na kitu fulani cha kujitambulisha nacho. Hawana budi kuwa na kitu fulani wanachotaka kufanana nacho, lengo fulani maishani.

Wanataka kuwa nyota wa sinema, ama kaoboi, ama—ama kitu kama hicho.

63 Nilikuwa nikisikia kwenye redio, nikija nyumbani, ambapo Mwitaliano fulani mashuhuri, huko Denver, alikuwa akijaribu kucheza Hopalong Cassidy, kitu fulani, na bunduki yenye risasi. Na badala yake, yeye atakuwa Chester, maisha yake yote. Alipiga risasi pia ya goti lake ikatoka. Haya basi.

64 Lakini wanajaribu kupata kitu cha kujitambulisha nacho. Sababu ya wao kufanya hivyo, ni kwa sababu kwamba kuna kitu fulani ndani yao, naye Mungu aliwafanya hivyo.

Lakini Mungu aliwafanyia mfano wapate kujitambulisha nao, na hapo ni wakati alipomfanya Yesu Kristo kuwa Mwokozi wako. Huyo ndiye mfano. Huyo ndiye watu wanayemtaka, wanaopaswa kutaka kutambulishwa pamoja na Yesu, kuwa kama Yeye.

65 Kama maskini wavulana wote wanaotaka kuwa Hopalong Cassidy ama—ama baadhi ya hawa wengine; ama hao wasichana wadogo, akina Annie Oakley na kadhalika; laiti wangalitaka tu kuwa kama Yesu, kadiri wanavyotaka kuwa namna hiyo, shule za Jumapili zingekuwa zimefurika, kila mahali. Kama wanawake wanaotaka kuwa kama bingwa fulani wa sinema, wangetaka kuwa kama Yesu, kanisa, mbona, kamwe haingewalazimu kuchukua sadaka. Hakika.

66 Mungu alimfanya mwanadamu kutamani kuwa na mfano. Ndipo Mungu akampa mfano. Mfano huo ni Yesu Kristo, kutambulishwa pamoja Naye.

67 Sasa, kama tungekuwa zaidi kama Yeye, basi kusingekuwako na wakubwa wengi hivi duniani. Kusingekuwako na watoto wowote wenye njaa ulimwenguni. Kusingekuwako na wiski yoyote, wala kunywa pombe, wala kucheza kamari. Mungu alitupa mfano wa kufanana nao, bali tunakataa kuwa huo. Sasa, hiyo ndiyo shida ya ulimwengu. Wana shauku, Mungu amewapa hiyo, bali wameigeuza vinginevyo. Wakati wa kurudi na kuingia kwenye njia ya kweli umewadia, na tuanze kuangalia Kalvari. Maumbile yanathibitisha hilo.

68 Sasa, kama watu wa siku hizi, pamoja na shauku hiyo kuu na kutaka makuu kuwa kama mtu mwingine, kama mfano. Kama walimchukua Kristo kama mfano wao, basi tungekuwa na. . .Tungeweza kumfuta kazi kila polisi aliyekuwako, nchini. Kila mtu angekuwa mpole na mnyenyekevu. Kila mtu angekuwa mwema na kuwa na upendano wa ndugu, mmoja kwa mwingine. Kamwe kusingekuwako na kisa cha kupiga talaka kilichowasilishwa mahakamani katika nchi yetu. Kamwe kusingekuwako na maradhi yoyote. Hata tungeziondolea mbali hospitali, kama kila mtu angejaribu kumfanya Yesu Kristo mfano wao. Tusingekuwa na haja ya kitu kingine chochote.

69 Kwa hiyo, asili hiyo iko ndani ya mwanadamu, bali anaiweka kwingine. Anamfanya mtu fulani. . .Nanyi mwajua, Biblia ilisema, ya kwamba, "Tumelaaniwa tunapoufanya mwili tegemeo letu. Unapojaribu kuufanya mwili tegemeo lako, ama kuweka matumaini yako katika mwili," Biblia ilisema, "umelaaniwa."

Jinsi ninavyojua hilo vizuri! Ni rahisi sana kufanya hivyo.

70 Hii ndiyo inayosababisha mengi yake, ni vibanda vyetu vya kuuzia majarida machafu; makazi yetu yamejaa picha zilizobandikwa ukutani. Skrini zetu za habari kamwe hazikaguliwi; zimefunguliwa wazi, zinaweza kutoa mizaha ya namna yoyote, ama—ama kufanya mambo ya kutisha. Hakuna usafi miongoni mwetu, tena. Ninajua mnafikiri mimi ni mkali sana juu ya hilo. Lakini ni. . .Mtu fulani anapaswa kuwa mkali kwake. Halina budi tu kufanywa.

71 Nilipokuwa mvulana mdogo, nilisoma kitabu cha *Tarzani, Masokwe*. Mama alikuwa na zulia la kale la manyoya ambalo Bi. Wathen alikuwa amempa, akaliweka mbele ya kabati la jikoni. Nilikatakata kitu hicho nikajifanyia suti ya Tarzani, na kulala juu ya mti kwa juma moja. Nilitaka kuwa Tarzani. Ndipo niliposoma kitabu cha *Mlinzi Mpweke Wa Nyota,* niliendesha mpini wa ufagio ukaisha, ukiwa ni farasi mdogo wa mbao, nikijaribu kuwa Mlinzi Mpweke wa Nyota.

72 Si zaidi ya vile watu watakavyofanya. Ni kile usomacho, muziki unaosikiliza.

Unaingia mkahawani, na maskini roki hii, si ajabu watu wanaingia kichaa. Hilo linatosha kumwingiza mwanadamu kichaa.

73 Lakini, loo, nitashukuru, kote katika Umilele, kwa siku moja niliposoma kumhusu Yesu. Hilo liliniridhisha. Ninataka kuwa kama Yeye. Hiyo ndiyo shauku yangu, kuweza kugeuza shavu hilo lingine, ama kwenda maili ya pili. Kuweza kusamehe, wakati mambo yamekuzidia, usiwe na neno dhidi ya mtu yeyote. Ingawa wanakutendea mabaya unavyostahili, ama usivyostahili kwa kutenda mema kwako, lakini hata hivyo wapende. Hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa. Ninataka kuwa mtu wa namna

hiyo. Ninataka kuweza, kwamba, wakati ninapotukanwa, nisitukane pia. Hiyo ndiyo aina ya mfano ambao Mungu alitupa katika Yesu Kristo. Tunapaswa kutambulishwa pamoja Naye. Tunatambu-. . .

74 "Je, unatambulishwaje pamoja Naye," ungesema, "Ndugu Branham? Sasa, kupata. . .inakubidi kuvaa kama mabingwa wa Hollywood na kufanya mambo haya mengine. Lakini unatambulishwaje pamoja na Yesu Kristo?"

Kwanza, unatubia yale uliyofanya tayari. Ndipo basi unatambulishwa pamoja Naye, hapa dimbwini. Hapana shaka ila wengi watatambulishwa pamoja Naye, katika dakika chache. Dimbwini, unatambulishwa pamoja Naye katika ubatizo. "Kwa kuwa kama tukizikwa katika Kristo, tunatambulishwa katika mauti Yake, kuzikwa, na kufufuka." Hiyo ndiyo sababu tunabatizwa. Tunaingia majini, tunatoka tupate kushuhudia ya kwamba tunaamini katika kifo, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu Kristo. Na kama tukipandwa katika sura Yake, katika mauti Yake, Mungu alitupa ahadi, tutakuwa kama Yeye, katika ufufuo.

75 Jitambulishe na malkia fulani wa sinema, uone mahali utakapokuwa. Jitambulishe na kaoboi fulani, ama tineja fulani, uone mahali utakapokuwa.

Ila nakupa changamoto, usiku wa leo, jitambulishe na Yesu Kristo, katika mauti Yake, katika kufufuka Kwake, uone mahali utakapokuwa katika ufufuo. "Kwa kuwa kama tukiteswa pamoja Naye, tutatawala pamoja Naye." Mungu ametupa ahadi. Shauku yangu yote ni kuwa kama Yeye.

Nichukue, Ee Bwana, na unifinyange na unifanye. Nichonge tena. Kama yule nabii aliyeshuka kwenye nyumba ya mfinyanzi, nivunje na kunifinyanga tena.

76 Katika Agano la Kale, wakati mtu anapotaka atambulishwe katika nyumba ya Mungu, alichukua kitu kisicho na hatia sana angaliweza kupata, mwana-kondoo. Naye alijua mwana-kondoo alikuwa huru na dhambi, maana hakujua dhambi. Naye akaenda, na kumchukua huyo mwana-kondoo, na kuweka mkono wake juu ya kichwa chake, na kukiri dhambi zake. Na kwa imani, akazihamisha dhambi zake juu ya yule mwana-kondoo, ndipo kutokuwa na hatia kwa huyo mwana-kondoo kukamrudia yeye. Halafu basi huyo mwana-kondoo akafa, kwa sababu alikuwa ni mwenye dhambi. Naye huyo mtu akaishi, kwa tendo la imani, la kutii aliyosema Mungu. Lakini yeye alifanya nini? Alitoka moja kwa moja hekaluni, akiwa na tamaa ile ile aliyokuwa nayo alipoingia. Kwa sababu, wakati seli hiyo ya damu ilipovunjwa. . .Ambayo, uhai huanza katika seli moja ya damu. Ndipo wakati seli hiyo ya damu ilipovunjwa, uhai wa huyo mwana-kondoo usingeweza kuingiana, ama kurudi katika uhai wa mwanadamu, kwa sababu ulikuwa ni uhai wa mnyama.

Mtu alitoka na shauku ile ile aliyokuwa nayo, kwa hiyo basi aliendelea kutenda dhambi, wakati wote, tena.

77 Lakini ulifika wakati ambapo Mungu alitutolea mfano, Naye akatupa Bwana Yesu. Basi mwenye dhambi anapoweka mikono yake juu ya kichwa Chake cha thamani, na kukiri dhambi zake, nazo dhambi zake zinabadilishwa ama—ama kuhamishwa kutoka kwa huyo mwenye dhambi hadi kwa Yesu; nako kutokuwa na hatia kwa Yesu kunahamishwa, na Roho Mtakatifu, kurudi ndani ya mtu huyo. "Yeye ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu." Hapo ndipo ninataka kutambulishwa. Biblia ilisema, "Yeye, pasipo kujua dhambi, alifanywa dhambi kwa ajili yetu." Sababu ya Yeye kuteseka ilikuwa ni kwa ajili ya dhambi zetu. Na si zaidi ya yaliyo kweli, jukumu letu si zaidi ya kuangalia vitu hivyo na kuona ya kwamba shauku hizi tulizo nazo, ambazo Mungu aliweka ndani yetu, kuumba ndani yetu, kutufanya kutaka kuwa kama Yeye.

78 Na sasa, kama unaweza kuliona, kwa imani, kabla shauku halisi kamwe haijapata kukugusa, njoo huku, utambulishwe pamoja Naye katika ubatizo. Halafu basi kwa kuwa umepandwa katika mfano wa mauti Yake, utashiriki pia katika sura Yake, katika ufufuo. Kwa kuwa wakati alipotoka kaburini, alikuwa ni Yesu yeye yule aliyeingia kaburini. "Na kama tukiwa ndani ya Kristo. . . " Tunaingiaje? Kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. "Kwenye siku hiyo tutatokea na kushiriki katika ufufuo Wake."

Kulikuwako na maskini wimbo mdogo ambao nilizoea kuimba, miaka mingi iliyopita:

Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha, kutoka duniani
  hadi Utukufuni,
Ninaomba tu kuwa kama Yeye.

Kutoka zizi la Bethlehemu alitokea Mgeni,
  (Mgeni, kwa ulimwengu.)
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha, kutoka duniani
  hadi Utukufuni,
Naomba tu kuwa kama Yeye.

79 Shiriki katika unyenyekevu Wake, utashiriki pia katika nguvu Zake. Shiriki katika utii Wake, nawe utashiriki katika kufufuka Kwake. Fanya jinsi Mungu alivyosema ufanye. Moyoni mwangu, jambo kubwa kuliko yote ninaloweza kuwazia, ni kuwa kama Yesu Kristo, kutambulishwa pamoja Naye. Hiyo hapo sababu ya mimi kuwabatiza watu katika Jina la Yesu Kristo, kwa sababu Yeye ndiye utambulisho wetu. Tunabeba ule utambulisho. "Kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, lifanyeni katika Jina la Bwana Yesu Kristo, mkimsifu Mungu kwake." Nasi tunatambulishwa pamoja Naye katika ubatizo.

80 Usiku wa leo, tutabatiza, katika dakika chache tu, watu hapa chumbani, walio hapa wapate kubatizwa. Na endapo kuna shauku yoyote moyoni mwako, kwamba unataka, una shauku yoyote kuu ya kilimwengu, zitubie hizo sasa hivi. Mwambie Mungu unasikitika ya kwamba ulitaka kuwa mtu fulani mkuu wa ulimwengu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Useme, “Bwana, shauku yangu kamili ni kuwa kama Yesu.” Njoo kwa upole, unyenyekevu. Halafu, unapoweka mikono yako juu ya Kichwa Chake, na kwa imani ukiri dhambi yako, useme, “Bwana, nasikitika nilifanya hivyo.” Basi itakuwaje? Mungu atahamisha hatia yako yote juu Yake, na kuchukua kutokuwa Kwake na hatia na kukurudisha juu yako. Nawe unasimama umehesabiwa haki, Mbele za Mungu, kwa sababu ulimwamini Yesu Kristo, Mwanawe. Ni mpango wa jinsi gani wa wokovu! Ndipo utashiriki katika utukufu Wake. Wema wa Mungu utaingia moyoni mwako. Nguvu za kufufuka Kwake zitakufanya mtu mpya. Zitaridhisha kila shauku.

81 Nilipokuwa mvulana, nilijaribu kufanya kila kitu. Ni—nilifanya kila kitu nilichokuwa mkubwa kutosha kufanya, na mambo mengi sana ambayo sikuwa mkubwa kutosha kuyafanya, nilijaribu. Nilikuwa nikipenda, ninapenda, kuwinda. Nilidhani hilo lilikuwa ndilo. Nilidhani kama mimi. . .Baba yangu alikuwa mpanda farasi. Nami nikawazia, “Laiti ningaliweza kwenda Magharibi na kuwafunza farasi wao!”

Lakini, ndugu, wakati mmoja huko juu nyuma kabisa kwenye milima ya Arizona, nikilitelemsha kundi la ng’ombe, usiku mmoja. Nilikuwa nimeketi pale. Ndipo mvulana aliyeitwa Slim alikuwa na kichanuo cha siku nyingi, pamoja na kipande cha karatasi juu yake. Alikuwa akicheza. Jamaa mwingine aliyeketi pale, kutoka Texas, akiwa na gita, akiipigapiga. Nao wakaanza wimbo. Nilikuwa nimetoa matandiko yangu kwenye farasi; nikakilaza chini kichwa changu, nikiyatumia kama mto. Nayo blanketi yangu imenifunika, nami mle ndani, na ningali nimevaa buti zangu, jozi ya vichokoo imeninyanyua ardhini. Naye akaanza kuipigapiga:

> Msalabani alipofia Mwokozi Wangu,
> Huko chini nililia nipate kutakaswa kutoka
>   dhambini;
> Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
> Utukufu kwa Jina Lake!

82 Nikajaribu kuivuta blanketi juu, na kuyafunga masikio yangu. Ningeangalia juu, nazo nyota zinaning’inia chini. Na hiyo misonobari inayochachatika milimani ilionekana kulia, “Adamu, uko wapi?”

Loo, kufuga ng’ombe kulikuwa ni jambo la pili. Nilitaka kumpata Mungu. Huko nyuma kabisa, nikapiga jozi ya hivyo

vichokoo, nikasema, “Bwana, sijui Wewe ni nani, lakini usiniadhibu mpaka ninapoweza kupata kitu kilicho halisi.”

83 Siku mbili baadaye, chini mjini, nikiketi kule, na baada ya siku chache baadaye, baada ya kuwakusanya ng’ombe. Nilikuwa nimeketi pale kwenye maskini benchi ya kale ya mbugani. Maskini msichana wa Kihispaniola akapitia hapo. Nami nilikuwa nimeketi pale, nikiwaza juu ya Mungu, “Ingekuwa ni nini?” Maskini msichana mdogo, akapitia pale, nami mvulana wa yapata tu miaka kumi na minane. Akaangusha leso yake na kupita. Nikasema, “Mwanamke, umeangusha leso yako.” Mawazo tu ya Mungu yalikuwa yamebadilisha shauku yangu. Maskini moyo wangu wa Kiairishi ulikuwa ukiona njaa, nilitaka kitu fulani, kitu fulani kilichoridhisha.

84 Mungu amenipa majaliwa ya kuwinda kote ulimwenguni: Afrika, India, kote milimani, Canada, kwenye baadhi ya safari zilizo kuu sana, na kuvunja rekodi za dunia. Yote, yote ni sawa, lakini hakuna kitu kitakachopachukua mahali pa nguvu hizo za Mungu aliye hai akishuka kuingia nafsini mwako.

85 Ninapofika kule, ninapenda milima. Ninapenda kutua kwa jua. Ni—ninapigilia tu kigingi, na kumfunga farasi wangu. Na kupanda, juu ya milima, na kukaa siku kadhaa, nikiangalia tu jua likichomoza na kutua, nikiwasikia tai wakipiga makelele. Ni kuzuri. Ninapenda kuwa kule. Ila, ndugu, moyo wangu unaanza kudundadunda na kupiga, ninapowazia juu ya,

> Mchafu! Mchafu! Pepo wachafu walimrarua.
> Yote ni mema Yesu anapokuja kukaa.

Ninaanza kuwazia juu ya wagonjwa, na mwito ule. Ndipo kuna kitu fulani ndani yangu, kinacholia, “Shuka kwenye milima hii upesi sana. Shuka kule kwa watu.”

Ninataka kujitambulisha mwenyewe kama mtumishi Wake miongoni mwa watu Wake. Loo, jinsi ninavyopenda kujitambulisha pamoja Naye. Halafu, kuhusu hilo, Yeye anarudi miongoni mwetu na kujitambulisha Mwenyewe pamoja nasi. Yeye yupo hapa usiku wa leo, rafiki.

86 Ni wakati sasa wa kuanza ibada ya ubatizo, katika yapata dakika kumi. Nami nataka kusema jambo hili moja kabla hatujaifanya, kabla hatujaanza. Yesu Kristo Mwana wa Mungu . . . Matamshi mengi tu ninayotaka kutoa, ila sina wakati.

Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, amejitambulisha Mwenyewe katika Neno Lake. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alijitambulisha Mwenyewe mkutanoni asubuhi ya leo, kwa kufanya upambanuzi. Hujitambulisha Mwenyewe katika kumleta mwenye dhambi kutoka katika njia za dhambi, akawa mtu mpya, kiumbe kipya. Humchukua mwanamke aliye duni kuliko wote ama mwanamume aliye duni kuliko wote, mlevi, mlevi sugu, na chochote kile, na kuwanyosha na kuwasafisha, na kuwafanya muungwana ama mama wa heshima. Huyo ni Bwana

wangu. Humchukua mtu aliye mgonjwa na anayeteseka, wala hamna matumaini kwake, na kumwinua kwenye maisha mapya tena. Kisha anaonekana miongoni mwetu, na kujitambulisha Mwenyewe kama Yesu yeye yule, kujua mawazo ya moyo wetu. Anasimama miongoni mwetu, katika watu Wake, Mungu ndani ya watu Wake, akijitambulisha Mwenyewe. Yeye yupo hapa sasa, Roho Mtakatifu yeye yule.

87 Kabla hatujaanza mkutano huo humu ndani wa ubatizo, wakati ndugu wakijiandaa, ninashangaa hili. Ninashangaa iwapo kuna yeyote hapa ambaye hakupata kuombewa, asubuhi ya leo, nawe ni mgonjwa. Hebu tuone mkono wako ukiinuliwa. Inueni mikono yenu kama nyinyi ni wagonjwa na wahitaji, wala hamkuombewa, asubuhi ya leo. Hakuna kadi za maombi wala chochote kile; wa—wagonjwa tu na wanaoteseka. Vema.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

88 Bwana, pamoja na koo hili lililojifunga, sauti iliyochoka, loo, ninaomba ya kwamba Wewe utaizamisha moyoni, ile Mbegu, kwa vyovyote vile, ndani ya moyo wa watu, tupate kutambulishwa pamoja Nawe. Kwa kuwa, ni methali ya kale hapa duniani, "Ndege anajulikana kwa manyoya yake, naye mtu anajulikana kwa wenziwe." Pia, mpendwa Baba wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa mwenzetu. Bwana, jalia tuwe Nawe, kama itagharimu kila kitu tulicho nacho duniani. Jalia tutambulishwe, kama, "Mtu huyo kweli anaishi pamoja na Mungu. Mwenziwe ni Mungu."

89 Jalia isemwe kama ilivyokuwa kwa Petro na Yohana, baada ya kupita kwenye Lango lililoitwa Zuri, na kusema, "Sina pesa zozote; lakini nilicho nacho, nitakupa." Ndipo yule kiwete akaponywa. Na wakati mbele ya mahakama, watu walisema waliona walikuwa wasio na elimu wala maarifa. Hawakuwa na elimu, bali waliona kwamba walikuwa wametambulishwa na wenzi wazuri. Walikuwa pamoja na Yesu. Mungu, hiyo ndiyo shauku ya moyo wangu, kutambulishwa pamoja na Wewe, kama mmoja wa watumishi Wako, kama mtu anayekupenda, mtu ambaye angekuwa mkweli Kwako, na kutii misemo ya Kitabu Chako, na kufanya yote nijuayo kufanya, hiyo ni kweli.

90 Sasa, Baba, naomba ujitambulishe Mwenyewe tena miongoni mwetu usiku wa leo, kusudi watu waweze kujua ya kwamba hiki si kitu fulani tu, loo, wakati maalum, ama—ama kitu cha namna hiyo, Bwana. Jalia ijulikane usiku wa leo ya kwamba Wewe ni Mungu yeye yule aliyekuwa hapa asubuhi ya leo. Una Nguvu zile zile. Na mambo yale—yale yale uliyofanya asubuhi ya leo, unaweza kuyafanya tena usiku wa leo. Uliahidi ya kwamba yatakuwa katika siku za mwisho.

91 Wengi hapa wasingeweza kupata imani ya kutosha. Tunaomba ya kwamba Wewe utawapa imani sasa. Pia jalia Roho Wako atambulikane miongoni mwetu, kwa kuwa Wewe

ulisema, "Kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya, aniaminiye Mimi." Kwa hiyo ninaomba, Mungu, ya kwamba utatambulisha ya kwamba Wewe upo hapa pamoja nasi usiku wa leo, na... ungali unatupenda. Nawe unamtaka kila mtu humu ndani, ambaye hajabatizwa, aje na kutambulishwa pamoja na Wewe. Ili kwamba wao pia waweze kuwa washiriki wa neema hii ya ajabu ambayo inaweza kuhamishwa; kutoka kwetu hadi Kwake, na kutoka Kwake hadi kwetu; hatia yetu Kwake, na neema Yake kwetu. Tujalie, Bwana. Yasikie maombi yetu, tunapoomba katika Jina la Yesu Mwanao. Amina.

92 Tumesimama kwenye kivuli cha haki ya Mungu. Kila wakati ambapo wawili au watatu wamekusanyika pamoja katika Jina la Yesu Kristo, Yeye aliahidi atakuwa miongoni mwao.

93 Sasa, sijui, nadhani sehemu ya kadi za maombi imechukuliwa. Baadhi yenu huenda mngali na zingine. Wengi wenu hamna kadi ya maombi. Haijalishi kama unayo au huna. Kama wewe ni mgonjwa, wewe ni mgonjwa. Na endapo... Mungu huyu aliyeiandika Biblia hii, mnamwamini kwa uchaji? Kama atarudi tena miongoni mwetu, kujithibitisha Mwenyewe, mbali na kuhubiriwa kwa Neno, ya kwamba Yeye yuko hapa, akiwashawishi wenye dhambi kwamba Yeye yuko hapa. kama Yeye yuko hapa kuwaponya wagonjwa, na atafunua asili yake, kama alivyofanya alipokuwa hapa duniani, kwa furaha utakubali uponyaji wako? Kama utaukubali, inua mkono wako, mahali popote tu. Hatutaninii...hatuna ninii...Nisingejua aliwapa kadi zipi za maombi. Hatutakuwa na kadi za maombi. Ninii tu, ombeni, na muamini.

94 Na endapo atafanya hivyo, na atajitambulisha Mwenyewe, inakupasa kujionea aibu kutojitambulisha pamoja Naye basi. Unapaswa kufanya hivyo. Sasa, hii hapa changamoto ya moja kwa moja. Kanisani asubuhi ya leo tulisambaza kadi za maombi, na kuwaita madhabahuni, na kuwaombea. Ndipo Roho Mtakatifu akatikiswa tukawa na wakati mzuri sana, mpaka nikawahisi wakinivuta pande zote, ilikuwa ni wakati wa kuondoka, kwa sababu nilikuwa mnyonge. Na sasa, hapa ninasema, ninyi msio na kadi za maombi, ama vyovyote mlivyo, mnaoketi huko nje kwenye kusanyiko, ninyi toeni changamoto. Nawapa changamoto kufanya jambo hili, kuamini ya kwamba hadithi niliyowaambia ya Yesu Kristo ni Kweli. Nanyi ombeni, endapo mu wagonjwa. Haidhuru...

95 Asubuhi ya leo, nilijaribu kuona kama ningeweza kuwapata watu ambao hawakuwa pamoja na maskani. Usiku wa leo, sijali mahali umetoka. Wewe omba tu. Ndipo kama huyo Roho Mtakatifu wa Mungu, tuliye na picha yake pale, laiti Yeye angalikuja miongoni mwetu! Mmenisikia nikihubiri hilo sana, kwamba Yeye alituahidi mambo, kwamba angefanya hivyo. Na halafu basi wakati alipokuwa duniani, wakati aliporudi katika

mwili wetu, Yeye angefanya jambo lilo hilo. Sasa, iwapo wewe ni mgonjwa, omba. Nawapa changamoto!

96 Mpe Mungu changamoto, useme, “Mungu, Ndugu Branham hanijui mimi. Hajui lolote kunihusu mimi. Lakini endapo utamjalia tu kunigeukia, uniruhusu kuligusa vazi Lako, kisha unene, nitajua ya kwamba Wewe una uhusiano na kanisa hili.” Kanisa ni waaminio. “Ndipo nitajua ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Nanyi muombe.

97 Ninajisikia tu kuongozwa kufanya hivyo. Sijui ni kwa nini nilifanya hivyo, lakini najisikia kuongozwa kufanya hivyo.

Sasa, kama utakiinua kichwa chako.

98 Papa hapa, akiniangalia, ni maskini yule mwanamke aliyeinua mkono wake namna *hii*, akiomba, dakika chache tu zilizopita. Naye anamwombea mtu mwingine mbali na yeye. Sijawahi kumwona mwanamke huyu maishani mwangu, nijuavyo mimi. Yeye ni mgeni kabisa kwangu. Bali anamwombea binti yake, kwa ajili ya upasuaji. Hata hutoki katika nchi hii. Umetoka Texas. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Una kadi ya maombi? Huna? Huhitaji moja. Amini kwa moyo wako wote.

99 Nilijuaje kile ulichokuwa ukiombea? Hivi huwezi kuona Mungu wa Mbinguni hufunua siri za moyo? Hivi Danieli hakusema hivyo katika siku zake? Mungu hufunua siri za moyo.

100 Kuna mama anayeketi karibu nawe hapo. Alikuwa na furaha sana juu yake. Alikuwa na ugonjwa wa moyo, naye anataka aombewe. Kwa hiyo kama utaweka tu mkono wako juu yake. Vema. Sasa, rudi Chicago na upate afya. Amina. Simjui mwanamke huyo, pia, sijui lolote kumhusu. Lakini Mungu anakujua. Unaona?

Yeye anajitambulisha Mwenyewe pamoja nasi. “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

101 Maskini mwanamke huyu wa Kiyahudi, anayeketi hapa, yeye alikuwa anaomba, pia. Hiyo ni kweli. Ulikuwa unaomba nikwambie jambo fulani. Niliyaona matatizo yako asubuhi ya leo, ila sikuyataja. Lakini miguu hiyo ambayo imekusumbua, itapona. Kwa hiyo usihofu chochote kuhusu hayo.

102 Unaamini, pia, maskini msichana unayeketi hapa? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Sikujui. Mungu anakujua. Lakini kama Yeye ni Roho wa Mungu pamoja nasi, basi atafanya kama Yesu alivyofanya. Ulikuwa ukiomba, na inaonekana kana kwamba nilivutiwa kwako. Huyo hapo Malaika wa Bwana karibu naye. Kama utaamini, ugonjwa wako wa moyo utakoma, na baridi yabisi. Jina lako ni Binti Wisdom. Hiyo ni kweli. Rudi na uwe mzima, Bi. Wisdom. Sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu.

Lakini, Yeye ni Mungu, ikiwa tu utaamini.

103 Hapa, angalieni hapa. Mnamwona yule mama anayeketi pale ameinua mkono wake namna *hii,* kinywani mwake? Kuna. . . Hivi hamwezi kuiona ile Nuru inayoning'inia juu ya huyo mwanamke hapo? Sasa, angalieni, inashuka moja kwa moja kwenda kwake. Ninaiona ikivunjika. Ana ugonjwa wa ini, anasumbuliwa na ugonjwa wa ini. Ni ugonjwa wa tezi kibovu. Vema, wewe ni Bi. Palmer. Jambo ndilo hilo. Ninakumbuka sasa ni nani. Sikuona, ni ono tu; ninakuona umeketi karibu na Ndugu Palmer. Hiyo ni kweli, dada. Sasa, nenda na uwe mzima. Amini, kwa moyo wako wote.

104 Kunaye maskini msichana anayeketi nyuma yake, pia, aliyeangalia juu, kidogo amestaajabu, papo hapo nyuma yake. Unafikiri matatizo ya findo za hao watoto wawili yataondoka, dada, nawe, pia? Basi nenda zako, nyumbani, na ushangilie na kuwa na furaha. Weka mkono wako juu ya hao watoto wachanga, wote wawili wenye matatizo hayo. Nalo tatizo lako liliondoka, pia. Mmeponywa, katika Jina la Bwana Yesu, ninyi nyote. Mtapona, mwe wazima.

105 Mnaweza kuona Mungu aliye hai yu hai leo hii? Yeye ni mkuu vile vile, mahali popote, sivyo? Hivi hamtaki kutambulishwa pamoja na Yeye? Bila shaka, mnataka. Hakika, mnataka kutambulishwa.

106 Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Kabla ya mimi. . .Hunidhoofisha sana. Ni wangapi wanaotaka kukumbukwa katika maombi sasa hivi, mkisema, "Mungu, unirehemu. Sasa ninataka kumwamini Bwana Yesu. Na—nataka shida zangu zote zinyoshwe sasa"? Mungu awe pamoja nanyi.

107 Bwana, Wewe uliyemleta tena Yesu kutoka kwa wafu, Mungu wa Mbinguni, ninakuomba Wewe, kwa niaba yao, ya kwamba hii itakuwa ndiyo saa ambayo wataamini; waje mbele, kama hawajapata kufanya hivyo awali, wapate kutambulishwa pamoja na Yesu Kristo, hapa kwenye dimbwi hili, usiku wa leo. Kwa kuwa Maandiko yalisema, kwamba, "Kama tukizikwa pamoja na Yeye katika ubatizo, na kushiriki na Yeye katika mauti Yake, pia tutashiriki katika ufufuo pamoja Naye." Hiyo ni ahadi. Naye yule Mtakatifu mashuhuri Petro, wa kale, alitwambia sisi, "Kutubu, na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nasi tutapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Juma hili lote. . .

108 Huyu hapa binti mkwe wangu ameketi, Bwana, maskini Loyce, akiona njaa, na kuona kiu, na kufunga, na kungojea. Yule pale dada yangu ameketi huko nyuma, akiona njaa, na kuona kiu, na kufunga, na kungojea. Ee Bwana, mtume Roho Mtakatifu sasa hivi kwa njia fulani, katika jengo hili, na kuzigusa nafsi zao kwa Nguvu za ufufuo. Na uwajalie kusimama kwa miguu

yao, katika Nguvu za ufufuo, na kutambulishwa pamoja na Yesu Kristo katika kufufuka Kwake. Tujalie, Bwana.

109 Samehe kila dhambi. Achilia ubaya wowote, Baba, na utupe neema Yako, tunapoomba katika Jina la Yesu Kristo.

110 Waponye wagonjwa wote na wanaoteseka. Bwana, Wewe uko hapa. Wewe ni Mungu. Wewe, Wewe hujithibitisha Mwenyewe, Mungu. Nasi tunaomba hayo, tukijua tabia ya Roho Wako, ya kwamba ulitenda mambo machache kisha ukatoweka kutoka kwao, ukaenda mahali pengine na kuingia kwenye mji mwingine, kisha ukaondoka na kwenda. Lakini uliacha alama nyuma, ya kwamba Mungu aishiye yu hai. Na mimi naomba, Bwana Yesu, ya kwamba—ya kwamba hii imekuwa ni mguso juu ya mioyo ya hawa watu, ya kwamba kamwe hawatasahau ya kwamba Roho Mtakatifu yupo apate kuponya, na kuokoa, na kujaza na wema Wake. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

111 Sasa, ni wangapi hapa walikuwa wabatizwe? Waweza kuinua mkono wako, uliyejiandaa. Mnaweza kujiandaa basi kwa ajili ya maji, katika dakika chache tu.

Na sasa wakati tukimngojea Roho Mtakatifu, kwa dakika chache tu. Ni wangapi hapa hawajampokea Roho Mtakatifu bado, nao wanatamani, wakiomba kwa bidii, kumpokea Roho Mtakatifu?

Teddy, ukiweza, ama baadhi yenu, kwenye piano, mara moja. Tutaimba baadhi ya nyimbo sasa hivi.

Wakati, wanawake wanaoenda kujiandaa kwa ajili ya ubatizo, nendeni kwenye chumba *hiki*. Nao wanaume waende kwenye chumba *hiki,* wanaojiandaa kwa ajili ya ubatizo. Tunapojiandaa, pia, kwa ajili ya jambo hilo.

112 Kisha tutamngojea Roho Mtakatifu kuja kwetu, na kutufunulia mambo ambayo anatutaka tufanye.

Halafu tutazima taa, katika ukumbi mkubwa. Mhudumu ataingia majini ha—hapa, halafu tu—tutafanya ibada ya ubatizo.

Hebu kidogo, kabla tu hujazima taa, Ndugu Evans. Ninataka kusoma baadhi ya Maandiko wakati tukingojea, kwa dakika moja tu, mkiweza. Wakati wakianza kujiandaa, ningetaka kusoma Maandiko fulani hapa.

113 Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Mungu hana kikomo? Hakika. Yeye yupo hapa sasa hivi. Jambo pekee likupasalo kufanya, kupokea Roho Mtakatifu, ni kusimama na kumkubali. Mbona, Nguvu Zake zimethibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa. Tungewezaje kuwa na tashwishwi hata moja? Uwepo Wake mtakatifu, uliobarikiwa ukiosha tu nafsi zetu! Ninajisikia kana kwamba ningeweza kupiga mayowe, kwa sauti yangu yote, kwa wema Wake. “Nazo rehema Zake zinadumu milele na milele.” Yeye yupo hapa. Moyo wangu unawaka moto, na umejaa shangwe na furaha nyingi, kwa sababu ya Uwepo Wake.

114 Kabla hawajazima taa, ninataka kusoma kutoka Matendo, mlango wa kwanza.

Nami ninaamini ya kwamba kila mtu, mhudumu, ama mtu aliye humu ndani, mwinjilisti, ama yeyote yule, ya kwamba kutakuwako na hili, kwamba, Mungu hana kikomo. Mungu hawezi kufanya jambo moja kwa njia moja, kisha ageuke na kufanya *hivi*, kulifanya—kulifanya vinginevyo. Hana budi kulifanya vile vile, kila wakati. Sivyo?

Haya ndiyo matangazo yaliyotoka kwa Mungu.

> *Enyi wanaume wa Israeli, sikilizeni maneno haya; Yesu wa Nazareti,* yule *mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa*. . .*maajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua:*

Yeye alifanya ishara za namna gani, kuthibitisha alikuwa Masihi? Kwa kujua mawazo mioyoni mwao. Hiyo ni kweli? Yale Petro aliyosema, "Kwa ishara na maajabu, Mungu alithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa pamoja Naye."

> *Mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa,* na *kwa kujua kwake tangu zamani, ninyi mkamchukua, mkamsulibisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua:*
>
> *Ambaye Mungu amemfufua, akiufungua uchungu wa mauti: kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao.*
>
> *Maana Daudi* alitaja *habari zake: Nilimwona Bwana mbele yangu siku zote,* . . .yuko *upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike:*
>
> Kwa hivyo mimi, *moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu* ulifurahi; *tena mwili wangu*. . .*utakaa katika matumaini:*
>
> *Kwa maana hutaiacha roho yangu katika kuzimu, wala hutamtoa Mtakatifu* wako *aone uharibifu.*
>
> *Umenijulisha* njia *ya uzima; utanijaza furaha kwa* nyuso zangu.
>
> *Waume na ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri* kwenu *habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo.*
>
> *Basi kwa kuwa ni nabii,*. . .*akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake ata—atamwinua Kristo* kuketi *katika kiti chake cha enzi;*
>
> *Yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho*

*yake haikuachwa kuzimu, wala* mwili wake *haukuona uharibifu.*

*Yesu huyu Mungu amemfufua,* hivyo basi *sisi. . .tu mashahidi wake.*

Loo, hilo linanichangamsha mimi! Sisi tungali tu mashahidi Wake. Yeye alifufuka katika wafu. Yeye yu hai, usiku wa leo.

*Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu,. . .akiisha kupokea kwa—kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia.*

*Maana Daudi hakupanda. . .*mbinguni, *bali yeye mwenyewe* alisema, *BWANA alimwambia Bwana wangu,* Keti *upande wa mkono wangu wa kuume,*

Mpaka *nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.*

*Basi nyumba yote ya Israeli wajue* yakini, *ya kwamba Mungu amemfanya Yesu* huyu *ambaye* nyinyi. . . *mlimsulubisha, kuwa Bwana na Kristo.*

Sasa, alikuwa akizungumza katika lugha gani, hata lugha hizo zote za ulimwenguni zikamsikia?

*Sasa walipoyasikia* (hao watu) *haya, wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na. . .mitume wengine, Tutendeje, waume na ndugu zetu*?

Muda mfupi uliopita walikuwa ni "wazimu" kwao. Sasa, baada ya mahubiri hayo mazuri sana yaliyokuwa yakitolewa kwa kila taifa lililosimama pale, "Tutendeje, waume na ndugu zetu?" Ndipo yakaja maagizo. Kisha maji-. . .

*Petro akawaambia, Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo, kwa ondoleo la* dhambi, *nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

*Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu,. . .kwa watoto wenu, na kwa* watu *wote walio* mbali, *na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.*

*Akawaambia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, Jiokoeni na kizazi hiki* chenye ukaidi.

Kama hiyo si Injili ile ile tunayohubiri siku hizi! "Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi." Ishara nyingi na maajabu yakifanywa, Uwepo wa Yesu Kristo akijionyesha Mwenyewe kuwa hai. Na ubatizo ule ule ulioagizwa papa hapa, umeagizwa papa hapa mimbarani, pia, usiku wa leo.

*Nao waliopokea neno lake kwa furaha wakabatizwa: na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*

115 Mungu mpendwa, hao, vyumba vimejaa watu waliosimama wakijitambulisha katika ubatizo pamoja Nawe. Ninakuomba

Wewe, Bwana, kwa niaba yao, ya kwamba kama utawafadhili tu, Bwana, kwenye wakati huu, watakapotoka majini, jalia jambo fulani liwapate, ili kwamba nafsi zao zitajazwa kwa Roho Mtakatifu. Jalia waje na waondoke majini, waende wakakudhihirishe katika kuhubiriwa kwa Injili, kufundisha shule ya Jumapili, kunena kwa lugha, kufasiri lugha, kufanya ishara, maajabu na miujiza, na, juu ya yote, upendo wa Mungu ukiwaka nafsini mwao, pamoja na upole, na unyenyekevu, na subira, na unyenyekevu.

116 Bwana, ninawakabidhi Kwako. Wao ni kumbukumbu za uamsho huu. Nami naomba ya kwamba Wewe utawaweka katika ulinzi Wako. Na siku moja . . . Kama ninavyosimama hapa nikiomba juu ya Biblia Yako, nikiisha kuhubiri kutoka Kwake, na kutangaza kwa moyo wangu wote yale ninayowazia kuwa ni Kweli, kama utakavyonifunulia mimi.

117 Na, Bwana, tunangojea ubatizo wao, kama vile sisi sote tulivyo katika hili kusanyiko hapa tukiungojea ufufuo. Ndipo siku moja, Bwana, wakati tukisimama pamoja katika mahali pa Mbinguni, jalia sauti itoke Mbinguni. Parapanda italia, nao wafu katika Kristo watafufuka, kwanza. Jalia tutwaliwe pamoja Naye, kumlaki Bwana hewani, na tuwe pamoja Naye milele. Tujalie, Baba.

118 Tuweke wenye afya, na wenye furaha, na tuliojaa bidii. Hatuombi pesa. Hatuombi mambo rahisi. Tunaomba tu kuwa kama Yesu. Tunataka kutambulishwa pamoja Naye, pamoja na Roho kama iliyokuwa ndani Yake, mpole, mnyenyekevu, sikuzote akifanya kazi za Baba yake.

119 Bwana, katika saa ya kumalizika kwa uamsho huu na huu utambulisho wa wengi wa watu wa thamani, endelea kujitambulisha Mwenyewe, kwa kuwapa Roho Mtakatifu. Tujalie, Baba.

120 Bariki maskani hii ndogo, bariki kila mhudumu, kila mtu ambaye ameuhudhuria, kila kanisa ambalo limekuwa hapa.

121 Bwana, ninaomba ya kwamba utatuma uamsho katika kila kanisa kote ulimwenguni. Nasi tutawaona wakija pamoja kwa moyo mmoja na nia moja, kwa ajili ya neema ya unyakuo wa Yesu Kristo tutakayopewa sisi. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

122 Sasa taa zitazimwa, kwenye sebule kubwa, kwa muda kidogo. Leso hizi zimeombewa. Na sasa taa zitazimwa kwa muda kidogo tu, halafu basi—halafu basi tunyamaze tu. Naye mhudumu atakuwa akibatiza, mmoja tu baada ya mwingine, mpaka tutakapowamaliza.

[Ndugu wanapanga fenicha upya jukwaani, katika maandalizi ya ibada ya ubatizo—Mh.] Sasa kama kila mtu anaweza kuona . . .

123 Sasa, na maikrofoni hiyo moja, vuta maikrofoni hiyo chini ya hilo tangi hapo. Naam. Hiyo ni sawa. [Mtu fulani anarekebisha kitegemezi cha maikrofoni—Mh.] Inaonekana bora zaidi. Naam. [Ndugu fulani anasema, "Hiyo ni ili kwamba tuweze kuunasa vizuri sana."] Hiki kinapeleka kwenye kinasasauti? ["Naam."] Vema. Yeye anashughulikia hilo.

124 Nilitaka kufanya jambo hili, mimi mwenyewe, usiku wa leo. Nina joto sana. Naye Ndugu Neville amekuwa akipumzika, kwa hiyo tunamtaka mchungaji awe na jambo la kufanya na hii, pia, ndugu mzuri sana.

125 Hebu kidogo, taa zitazimwa, kwenye ukumbi mkubwa, ndipo mtaweza kuona, kwa glasi kubwa inayonig'inia nyuma yake, inayoelekea moja kwa moja katika dimbwi ambamo watakuwa wakija, kubatiza, mara watakapowatayarisha.

126 Na kila wakati, wanapobatiza, wataninii . . . wazee watafunga hilo pazia. Hiyo itafanya . . . kwa ajili ya wanawake, wanapoingia na kutoka majini. Na kwa hiyo basi watakuwa wakija, mmoja mara baada ya mwingine. Utasema jina lako, useme wewe ni nani, na kuwabatiza katika Jina la Yesu Kristo.

127 Sasa, kumbukeni, kama—kama tu mhudumu, anayewajibika kwa Injili hii niliyokabidhiwa, ningeipendekeza kwa mtu yeyote ambaye hajabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, ubatizwe tena. Hivyo ndivyo Paulo alivyosema. Hata wakati huo, walipokuwa wamebatizwa kwa njia moja, pasipo na Jina, yeye alisema itawabidi kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo.

128 Alisema, "Kama Malaika akija, afundishe kitu kingine chochote, na alaaniwe." Hilo linapatikana katika Wagalatia. Wagalatia, mlango wa kwanza, na kifungu cha 8. "Ijapokuwa sisi, au Malaika kutoka Mbinguni, akihubiri injili nyingine yoyote, na awe kwenu aliyelaaniwa."

[Pazia la mahali pa kubatizia linafunguliwa—Mh.]

129 Sasa, kabla tu ya ibada kuanza, kila mtu anaweza kuona? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . akashuka katika maji ya mauti. Sasa tunajiunga na wahudumu wa Injili, hapa sisi . . . ? . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] Rafiki msiri wangu sana, kutoka huko chini . . . ? . . . Mama huyu ni rafiki msiri wa Oral Roberts; yeye na mume wake . . . ? . . . askari mwingine mkuu, mwenye kuwavuta watu wengi kwa Mungu, Ndugu Oral Roberts, mmoja wa marafiki wasiri wangu, pia. [Sehemu tupu kwenye kanda.] Naam.

59-1220E Kutambulishwa Pamoja Na Kristo
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org